# *Kufanya Mlango*

Habari za jioni, marafiki. Na Bwana awabariki sana.

Na asante, Ndugu Neville, kwa kutoa hayo matamshi mema. Nina furaha sana kurudi kwenye maskani usiku huu, katika utumishi wa Bwana wetu aliyebarikiwa, na kuwaona marafiki wetu wametoka, usiku wa leo, na kumwabudu Yeye pamoja nasi.

2 Bila shaka ni majaliwa mazuri kukutana tena upande huu wa Kuja kwa Bwana. Baada ya kuona, kusikia, wengi sana wakiaga dunia, bila kutarajiwa, upesi sana, tunashangaa tu, wakati baada ya wakati, ni nani atakayefuata. Lakini, tukiwa na dhamana hii iliyobarikiwa, ya kwamba kama . . . "hakuna kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo. Hakuna mauti, wala—wala mambo yaliyopo, wala hakuna mambo yajayo, wala mamlaka yo yote, yanayoweza kututenganisha na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu." Na kujua jambo hili, ya kwamba, "Nyumba ya maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja inayotungoja tayari." Bila makao, bila starehe; na tunategemea tumaini hilo lililobarikiwa na lenye utukufu sana.

3 Nilikuwa nikizungumza na mke wangu, na Bibi Woods na hao wengine, kuninihii tu . . . niliporudi. Nilikuwa ninasema, "Vema, inaonekana tu kama kwamba ni safari baada ya safari, na mahali baada ya mahali, lakini, hata hivyo, inakuwa yenye utukufu zaidi. Nami . . . nikijua ya kwamba tunafikia mwisho, kule—kule—kule kukaribia kwa Kuja kwa Bwana." Nikasema, "Vema . . . "

4 Nikizungumza na mvulana wangu, tulipokuwa tunakuja barabarani juzijuzi, tukitoka kwenye Sioux Falls, Dakota ya Kusini. Ndipo nilisema, "Wajua, nyumbani ni mahali pazuri sana." Tulikuwa tukirudi nyumbani. Nikasema, "Tunaupenda ulimwengu huu. Huu ndio makao yetu. Huenda tusifikiri ndio makao, ndio. Tulizaliwa kwa ajili ya makao haya. Hapa, Mungu alituweka hapa. Hatukuwa na njia ya kujileta hapa. Hata baba yetu na mama yetu hawakuwa na njia. Hilo lilibidi liwe mikononi mwa Mungu. Watu wengi wamefanya ndoa, hawajapata kupata mtoto. Lakini, Mungu aliona ya kwamba tungekuja katika dunia hii.

5 Ndipo tulipokuja, tulianza kukua na kuumbika katika mwili, kwa atomi na nuru, na kadhalika, ulipoanza kuchukua kutoka duniani. Ndipo tulipofikia umri fulani, ikaacha kukua. Tungali tunaongezea kwayo, bali inaondoka. Mauti yameingia.

6 "Na nyumba ya maskani maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunalo jengo lingine kule likingoja." Mnaona? Tunaingia kwenye huo, tutajuana sisi kwa sisi. Hatuwezi

kupeana mikono; hatuna hisi za kule kujisikia. Hatuwezi. . . Nisingeweza kukupa mkono, kusema, "U hali gani, ndugu," kwa maana mimi—mimi. . .usingekuwa na mkono wa namna hiyo. Lakini, hata hivyo, hatuko katika mwili wa nyama kama tulivyo sasa, tuko katika mwi—mwili wa kimbinguni. Halafu wakati huu. . .

7 Nami nilikuwa nikiwazia, ya kwamba kule Misri, ya kwamba wakati Yusufu alipoacha kumbukumbu fulani, kwa wana wa Israeli, mifupa yake, ya kwamba siku moja watatoka. Nao watakapokuwa wanatoka, wangechukua mifupa yake, waipeleke kwenye nchi ya ahadi. Na kila Mwebrania aliyetamani kurudi kwenye nchi ya uenyeji wao, kwa hiyo haidhuru alitendwa vizuri namna gani, hata hivyo hamu yake ilikuwa ni kurudi kwenye nchi ya ahadi. Na kila wakati walipopita pale na kuona mifupa hiyo, walijua ya kwamba siku moja watarudi kwenye nchi ya uenyeji wao.

8 Wakati tukiwa hapa, tukingojea kuvuka tutoke mahali hapa, tunaona kaburi lililo wazi kule Yerusalemu, linatufanya tujue ya kwamba jambo fulani lilitukia. Ndipo tutakapoichukua hiyo iliyotukuzwa. . .si iliyotukuzwa, bali mwili wa kimbinguni, na tunatembea kila mahli katika nchi zenye Utukufu pamoja na Kristo, tukiangaliana, tukizungumziana; tunaweza kuzungumza. Nafsi zilizo chini ya madhabahu, zikilia, "Hata lini?" Na basi hilo litakuwa kumbukumbu pale, ya kwamba tunarudi duniani tena kula na kunywa na kulala. Atakuwepo pale, ameketi kwenye Kiti cha Enzi, katika mwili wa nyama. Amina.

9 Siku moja Yeye atafufuka, katika mwili huo wa nyama. Na wakati atakaporudi, miili hii ya kimbinguni itatukuzwa. Ndipo tutakuwa kama Yeye, na tutaishi milele katika mwili huo. Ni ninii jinsi gani. . .Jambo—jambo lingine lo lote linajalisha nini? Mnaona? Yote yamekwisha tayari. Hilo ni ninii tu. . .Jitie nanga papo hapo. Na hebu huu. . .

> Tumaini langu halijajengwa juu ya cho chote
> Ila Damu ya Yesu na haki Yake;
> Wakati yote yanayonizunguka yanapovunjika,
> Wakati huo Yeye ndiye tumaini na nguvu zangu
> zote.

10 Kristo ndiye aliyefanya jambo Hilo liwezekane; si kanisa langu, wala si madhehebu yangu, si rafiki zangu, bali ni Kristo.

> Mahali pengine po pote ni sakafu ididimiayo,
> mahali pengine pote.

11 Si ajabu Eddie Perronet. . .Wao walifikiri alikuwa mwenda wazimu. Na siku hiyo, huku ameketi pale kama mtumwa kwa hao watu, Roho Mtakatifu alichukua kalamu akaanza kuandika huo wimbo mzuri sana utakaoimbwa kwenye ibada

ya kupandishwa cheo ya kutawadhwa kwa Mfalme wa wafalme: *Wote Na Waishangilie Nguvu ya Jina la Yesu.*

12 Taarifa nzuri sana kutoka kaskazini sasa. Tulikuwa na kifungua kinywa cha, si cha wahudumu, bali cha Wafanyi Biashara Wakristo kwenye. . .kule Minneapolis, na kifungua kinywa kikubwa sana tulichopata kuwa nacho cha wafanyi biashara. Watu elfu mbili walitoka wakaja.

13 Naye Bwana akatupa Ujumbe. Na asubuhi hiyo, katika wito wa madhabahuni, wafanyi biashara hamsini walimjia Kristo na wakazaliwa mara ya pili, asubuhi hiyo kweye ibada. Loo, hilo liliufurahisha sana moyo wangu, wafanyi biashara wakiingia! Ibada za ajabu, kila mahali. Bwana asifiwe, na utukufu wote Kwake!

14 Na sasa nina muhtasari mdogo hapa, kasema, "Nitakuwa Indianapolis lini?" Tarehe 11 hadi 15 Juni, nitakuwa kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis Indiana, tarehe 11 hadi 15 Juni, inayotoshea watu kumi na moja elfu.

15 Kesho kutwa, tutaondoka kwenda Shreveport, Louisiana, na tuwe kule mwishoni mwote mwa juma huko Shreveport, Louisiana.

16 Ndipo tutaondoka Shreveport kuelekea Houston, Texas, nasi tutakuwa kule siku mbili, ambazo zitakuwa ni Jumatatu na Jumanne.

17 Halafu tarehe 16 tutaanza huku Mexico ya kale, Jiji la Mexico, Mexico ya kale. Bw. Arganbright ndiyo kwanza aniite. Nao wamepata uwanja mkubwa wa dume kule, ambao unawatoshea watu sitini elfu walioketi chini. Na kuna makanisa mia nne yanayoshiriki, yaliyojiandikisha tayari. Tunatarajia laki moja mkutanoni.

18 Na ni mara ya kwanza jambo hili. . .Tuna jambo la kumshukuria Mungu. Mara ya kwanza katika historia ya Mexico, ambapo serikali imepata kumkaribisha Mprotestanti na kutupa mahali pa kuja. Mara ya kwanza katika historia ya Mexico, M—Mprotestanti amepata kukaribishwa. Na huyo Generali Valdivia, ni Jenerali wa jeshi la Mexico, ndiyo kwanza azaliwe mara ya pili na kupokea Roho Mtakatifu. Na kwa heshima yake kwa gavana wa Mexico, tumepewa haki ya serikali kuingia kule huku tunalindwa na jeshi. Na kwamba sisi tuna-. . .

19 Nimepata ule wanja mkubwa wa michezo ya dume. Huo ndio ulio mkubwa sana katika Mexico nzima. Unatoshea watu sitini elfu waliioketi, kuuzunguka namna hii, mbali na e—eneo wanamopigania, mwajua, kule ndani. Nasi tuliupata kwa siku kumi usiku mfululizo. Moja kwa moja siku kumi usiku mfulilizo. Mwe mkiniombea.

20 Ninajisikia tu...ninasikia sauti ya mvua kubwa kule. Nina ninii tu...Wamexico ni waumini rahisi sana, wanyenyekevu. Na mara wanaposhawishika...Wao ni Wakatoliki. Na mara wanaposhawishika ya kwamba Kweli ni kweli, basi hilo linatosha kwa yote.

21 Halafu, nikirudi haraka kutoka Mexico ya kale, nitarudi hapa kama tarehe 30.

22 Na ya kwanza, hiyo ni asubuhi ya Pasaka, kwenye maskani hapa, kwa ajili ya ibada ya alfajiri. Na ibada ya kuponya, kuifuata hiyo. Na ibada ya ubatizo usiku huo, maskanini. Nanyi mnaweza kuwaambia marafiki zenu, sasa, kuwaleta wagonjwa wao wote na walioteseka, kwa ajili ya ibada ya Pasaka. Ibada ya alfajiri asubuhi hiyo na mapema. Halafu, baadaa ya jambo hilo, kwenye saa nne, saa tatu na nusu ni wakati wa shule ya Jumapili kama kawaida. Nyote fanyeni mpango, shule ya Jumapili. Na—na ibada ya kuponya kufuata hiyo, ninii...ibada ya kawaida ya kuponya kama tunayokuwa nayo kwenye kampeni.

23 Na halafu, basi, Jiji la Mexico litakuwa ndiyo mara ya kwanza ambapo ono hili jipya, ambalo Bwana ameniambia habari zake, litakuwa likitenda kazi wakati huo. Kwa hiyo tutajaribu tena, Bwana akipenda, papa hapa, asubuhi ya Jumapili ya Pasaka, tukitumia vyumba hivi viwili,...?...hapa, mnaona. Kwa hiyo tunatarajia wakati mzuri sana hapa, asubuhi ya Pasaka.

24 Na thibitisho ya kwamba Bwana Yesu amefufuka katika mauti, Yeye yu hai. Naam, bwana. Naye amekuwa hai tangu ile Pasaka ya kwanza. Naye yuko hapa pamoja nasi hata sasa. Nami natumaini tu ya kwamba Bwana atatupa kumwagiwa kwingi kwa baraka Zake kwa ajili ya asubuhi hiyo.

25 Kisha tutaenda, kutoka hapa basi, tutaenda Chicago, kwa ajili ya ule wa tarehe 11, 3 mpaka 11. Nasi tunaondoka Jumatatu, tuanzie kule Jumanne, na kuanzia kwenye...La, ni tarehe tatu mpaka 8. Halafu tarehe 11 tunaanzia Charlotte...La, Columbia, Carolina ya Kaskazini. Halafu tuende Spindale, Carolina ya Kaskazini. Ndipo, kutoka huko, tuende Charlotte, Carolina ya Kusini. Halafu Anchorage, Alaska, kutoka huko; mpaka Anchorage, Alaska. Halafu, turudi. Na sijaazimia, lakini, labda, huenda ikawa kwenye wakati huo, ile hema itakuwa tayari kuanza safari. Loo, ninaninii tu...

26 Mnajua ninalotaka kufanya? Mtaomba pamoja nami kwa ajili ya jambo hili? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Angalia. Ninataka, karibuni, Bwana akipenda, kuweka hema hiyo papa hapa katika Fall City, na kukaa kule kwa ajili ya mkutano wa majuma manne ama sita; kukaa tu papa hapa mpaka vita vitakapokwisha. Nanyi mwe mnaombea jambo hilo sasa. Nami ningependa tu kuiweka katikati ya Jeffersonville na New Albany mahali fulani, na kuweka tu ya kukaa yapata

watu elfu saba ama nane ndani yake. Halafu tunaweza kuongeza wengine siku zinavyoendelea, na kukaa tu papa hapa mpaka imekwisha. Amina.

27 Halafu, basi, nafikiri basi tarehe 11 mpaka 15 Juni, kwenye Maskani ya Cadle huko Indianapolis. Halafu, tarehe 17, naamini, mpaka 21 Juni, itakuwa Minneapolis, kwenye uwanja wa mpira kule, unaotoshea watu ishirini na saba elfu. Huo ni mkutano wa kimataifa wa Wafanyi Biashara Wakristo, nikihubiri, na kuwaombea wagonjwa kila usiku.

28 Na sasa iweni mkiomba juu ya mambo haya, tafadhalini, ombeni sana. Na—najisikia tu ya kwamba hatuna wakati mwingi sasa. Nami nabashiri; sisemi huyu ni Bwana anayesema jambo hili sasa. Nina—ninabashiri ya kwamba mwaka huu Marekani aidha itampokea Kristo ama itamkataa Kristo. Mnaona? Ninaamini huu utakuwa ndio wakati wa maamuzi, ambao Marekani itaingia. Aidha tutakuwa na ufufuo katika siku hii, ama hatutakuwa na ufufuo. Na ninaamini huu ndio mwaka ambao Marekani itafanya maamuzi yake. Nami natumaini ya kwamba wao wataamua nasi tutakuwa na ufufuo mkubwa ambao utaenea tu. Tuna kuhubiri kwingi, na uijilisti mwingi, bali tunahitaji ufufuo (sivyo?), ufufuo halisi. Huo ndio tunaohitaji. Bwana awabariki.

29 Nafurahi kumwona Ndugu Graham pale, na—na—naamini Ndugu Smith ameketi papo hapo mbele yake, Ndugu Smith kutoka kwenye kanisa la Mungu. Na—na kuna wahudumu kadha hapa, nina hakika. Nasi tunawakaribisha nyote, enyi ndugu, kila mmoja, na wageni malangoni mwetu, washiriki wote. Tunawapenda sana.

30 Na sasa baada ya kumaliza matangazo haya, na nikitambua ya kwamba usiku huu, usiku wa ushirika kwa ajili ya ibada ya ushirika. Na mumwombee sana Ndugu yetu mpendwa Neville ambaye anashikilia ngome hapa maskanini, akifanya kazi nzuri sana; na kwa ajili ya watakatifu wote kila mahali. Loo, ni wakati wenye haja namna gani! Ni wakati wenye haja namna gani! Ninasikia jambo hilo kutoka kule Afrika, na mwito kama huo kwa ajili ya Afrika.

31 Na Ndugu Arganbright alikuwa akiniambia hivi punde tu kwenye simu, muda kidogo uliopita, ya kwamba mfalme wa—wa baadhi ya nchi hizo kule, ninasahau ilikuwa ni wapi. Ninaamini ni hapa Sweden, Switzerland. Nitalipata katika muda kidogo. Denmark, ame—ameandika barua maalum nijaribu msimu huu kwenda kule wakati huu.

Katika Afrika na India, mahali pengi mbalimbali!

32 Ambapo, visiwa vya Hawaii viliingia juzijuzi. Hiyo ni kama mara ya kumi moja kwa moja ambapo wamepiga simu kwa ajili ya ufufuo. Wafanyi Biashara Wakristo wanataka kwenda kule

na kuruka tu juu yake, waratibishe, waanzishe ushirika nami niwahubirie asubuhi hiyo, halafu ufufuo uanze Hawaii.

33 Kwa hiyo, ulimwengu mzima umekuwa mtaa wetu, mnaona, ulimwengu mzima. Nasi ni watumishi wake.

34 Kwa hiyo hebuni tu tukumbuke, enyi marafiki, ya kwamba huu huenda ukawa ndio usiku wa mwisho, huu huenda ukawa ndio mwaka wa mwisho, ama huenda ukawa ndio kizazi cha mwisho. Mnaona? Hatujui. Lakini, hata hivyo, tunajua kweli hii, ya kwamba walio hai wanajua hawana budi kufa. "Watu wamewekewa kufa mara moja, na baada ya kufa Hukumu." Na kama kungekuweko na ye yote hapa usiku wa leo, ambaye hako tayari kukabiliana na jambo hilo, wala hana tumaini hili lililobarikiwa, na usiku huu uwe usiku ambapo utaamua kumfuata Bwana Yesu, mara moja tu, hata Milele.

Na tuombeni sasa.

35 Baba yetu wa Mbinguni, tunataka kukushukuru Wewe kutoka kwenye kilindi cha mioyo yetu, tukijua ya kwamba tunangojea hapa, bila kuhangaika hata kidogo; haidhuru watatengeneza mabomu mangapi ya atomiki, na ni wafanyi kazi wangapi wa serikali watawaweka kule kuchunguza zile ndege, ulimwengu una wasiwasi na unatetemeka. Tunategemea tumaini hili lililobarikiwa tulilo nalo. Tunatumaini katika kazi ya Mungu iliyokwisha pale Kalvari, kwa njia ya Kristo. Tukijua jambo hili, ya kwamba baada ya maskani iliyo ya dunia hii kwisha, tunayo nyingine inayongoja kule ng'ambo; iliyo na utukufu zaidi, zaidi sana, ambapo hapana uchungu wala mateso, wala ugonjwa. Hakuna wakati wa uzee utakaoufikia, hapana hata unywele mmoja wenye mvi, hakuna hata kunyanzi moja, bali tutakuwa vijana kule milele.

36 Biblia iliyobarikiwa, ambayo haiwezi kusema kitu ila kweli, imetupa dhamana hii iliyobarikiwa. Naye Roho Mtakatifu, pia, ni shahidi, akishuhudia jambo lile lile. Mioyo yetu inatamani jambo hilo. Nasi tunajua Biblia inatuambia jambo hilo, ambayo ni Neno la Mungu, mbegu zipandwe kwenye ardhi hii iliyo na rotuba tupate kustarehe katika tumaini hili.

37 Mungu, naomba ya kwamba Wewe utamgusa kila mtu usiku wa leo, nje ya Kristo. Na kuwaleta kwenye kutembea huku kwa karibu na kuzuri sana. Waponye wagonjwa wanaoketi hapa usiku wa leo, Bwana. Hapana shaka, katika watu hawa wengi, hapana budi pawe na magonjwa kati yetu. Nasi tunaomba ya kwamba utamponya kila mmoja.

38 Sasa njoo kwenye Neno, Baba. Chukua Neno ambalo ni kamba ya uhai. Mizizi, Bwana, ya ustaarabu wote. Tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atachukua kila Neno na kulitia moyoni kulingana na haja zetu. Na tushiriki kwenye Neno. Kwa maana tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

39 Kwa ajili ya kusoma kidogo kwa Maandiko, usiku wa leo, kwa ajili tu ya fu—fungu ndogo, kujaribu kutafuta yaliyomo, kisha tuingie haraka moja kwa moja kwenye Neno, ili tupate kuwa na ushirika. Kwa kuwa kesho ni Jumatatu, najua hatupendi kufikiria mambo hayo, ya kulazimika kurudi kazini, bali hatuna budi kukabiliana na jambo hilo. Na wakati mwingi, mwajua. . . Lakini, hata hivyo, huu ni muhimu sana kuliko kazi na cho chote kile. Mnaona? Kwa kuwa, kazi yako itakwisha, siku moja, nawe utakwisha pamoja nayo. Bali kama ukiwa na Uzima wa Milele, hutakuwa na mwisho kamwe. Ni wa Milele; utaendelea kuishi, daima. Wazia jambo hilo. Uzima wa daima, hauna mwisho. Wakati wakati usioweza kupimika umepita, wewe utakuwa ungaliko. Wakati mamilioni ya miaka yatakapopita, tutakuwa tungaliko. Kwa hiyo, kwa siku chache tu hapa duniani, kazi hazina faida sana. Ni za kutusaidia tu tunapoendelea, kununua chakula chetu kidogo, na kadhalika, kula, ambazo hatuna budi kuwa nazo.

40 Sasa katika Wakorintho wa Kwanza sura ya 10, kuanzia aya ya 12.

> Basi *anayejidhania kuwa amesimama na aangalie* asije akaanguka.
>
> *Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye* si. . . ambaye—ambaye hataki m-. . .*hatawaacha mjaribiwe kupita* vile *mwezavyo; lakini*. . .*pamoja na* kila *jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*

41 Ni aya nzuri jinsi gani! Bwana na aongeze baraka Zake kwake. *Kufanya Mlango,* ndilo ningetaka kuzungumzia, usiku wa leo. Kujua. . . Na aongeze baraka Zake kwenye Neno Lake, tunapolisikiliza Neno sasa.

42 Ni maoni yangu, ya kwamba kama Neno, ambalo ndilo mizizi, ambayo ndicho kitu kinachoshikilia. Mara nyingi katika ibada zangu za kuponya, mimi—mimi hujaribu, hata baada ya waalimu kupitia jambo hilo lote, mimi hujaribu kurudi na—na kulichukua Neno na kuweka msingi.

43 Siku chache usiku zilizopita, nilipata barua ndogo ya kukosoa, jambo ambalo ni sawa. Mtu fulani aliniambia, kasema, "Ndugu Branham, wewe ni mvulana tu, bado." Kasema, "Nilikuwa nikihubiri Injili kabla hujazaliwa." Kisha akasema, "Mimi. . . Miaka yangu yote arobaini na sita, lakini hata hivyo. . . " Yeye—yeye alikuwa mwalimu wa shule fulani ya Biblia. Akasema, "Lakini mtu, wa namna yako, ambaye huwafundisha watu, na hata hivyo angetoa tamshi kama lile ulilotoa juzi usiku." Kasema, "Nafikiri ni upuzi." Kasema, "Ulisema Ibilisi hakuwa na nguvu za kuponya." Akasema, "Labda, vipi kama ningekwambia ya kwamba Ibilisi ana nguvu za kuponya." Akasema, "Sasa ungeniuliza, kama ulikuwako,

jinsi ninavyojua." Kasema, "Nitakwambia." Kasema, "Katika mji wetu, kuna mwanamke anayeishi kule ambaye ana roho m—mchafu. Naye . . . Watu humjia wapate kuponywa." Anasema, "Yeye atang'oa nywele kichwani mwao, kisha atatoa damu kutoka kwenye vena zao, na kuifunga kwa nywele hizi. Ataenda zake mtoni, na kutupa kitu hiki juu ya mbega lake, wala hataangalia nyuma. Kama akiangalia nyuma," kasema, "basi huo ugonjwa unabaki na mtu huyo. Lakini hana budi kuitupa mtoni, kana kwamba ilikuwa ni msamaha, kisha anaenda zake." Kisha akasema, "Asilimia sitini ya watu, tuliwahesabu, wanapona." Kasema, "Sasa, kama Ibilisi hawezi kuponya, na hayo je?"

44 Kwa, hiyo nikamjibu. Nikasema, "Ndugu yangu mwema na mpendwa, kwa heshima yote inayostahili miaka yako," unaona, "heshima yote ya miaka uliyofundisha, lakini nitakwambia sasa ya kwamba Yesu Kristo alisema ya kwamba Ibilisi hana nguvu za kuponya. Na kama Yesu alisema jambo hilo, hilo latosha, kwangu. Yeye Alisema, 'Kama Shetani akimtoa Shetani, basi ufalme wake umegawanyika na una mwisho. Wala hawezi kumtoa Shetani.' Ndipo ungeniuliza mimi, 'Kwa nini watu hawa wakaponywa?' Mbona, si mtu huyo. Huyo mchawi hakuwa na uhusiano wo wote na jambo hilo, si zaidi na vile mimi ningalikuwa na uhusiano wo wote nalo, wala mtu mwingine ye yote. Ni hao watu wanaokaribia, wakifikiri ya kwamba wanakuja kwa njia iliyoandaliwa na Mungu ya kuponywa kwao. Ni imani yao ya kibinafsi katika Mungu, ambayo huwaponya. Mnaona? Hiyo ndiyo njia wanayofikiria. Si huyo mchawi, si zaidi ya vile ingalikuwa mtu huyo." Naam.

45 Kwa hiyo, basi, Injili inaweza tu kwenda, ama inaweza tu kwenda jinsi Neno la Mungu linavyofundishwa. Nao watu wanawekea tumaini lao msingi katika Neno la Mungu Milele. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno."

46 Dk. Adair, hapa jijini, ndugu yangu mpendwa, aliniambia siku moja, akasema, "Billy, hivi hufikiri kama watu walikuwa na imani kuugusa mti ule kule, wangepata matokeo yale yale?"

47 Nikasema, "Ungewezaje kuwa na imani katika jambo hilo? Kama ungeweza kuwa na imani kiasi hicho hicho, kuamini . . . kuamini ya kwamba ilikuwa ni njia iliyoandaliwa na Mungu, kwako kuuguza ule mti, na ingefanya hivyo, basi wao wangeweza kufanya hivyo. Lakini ni nani aliye na imani katika mti huo?"

48 Nina imani na yale aliyosema Mungu, nami nachukua hayo tu. Kwa hiyo imani hainjengwi juu ya changarawe inayodidimia ya—ya mawazo ya miamsho. Lakini imani imenjengwa juu ya kanuni, Neno la Mungu la Milele, Mwamba wenye imara. Hapo ndipo imani inapochukua msimamo wake wenye uchaji wala haitikisiki, inapojengwa papo hapo.

49 Sasa, kufanya mlango. Mimi siamini ya kwamba Mungu huendeleza shughuli zake vivi hivi. Ni—nisingeendeleza zangu, wewe usingeendeleza zako. Yesu hakufa pale Kalvari kusudi aseme tu, "Vema, sasa labda watu watanisikitikia, kwa kuwa nimekuja, nimeenda duniani na kuchukua mfano wa mwili. Nao kweli wataokoka, labda, kama wakiona jinsi nitakavyokufa kwa huzuni." Mungu hakufanya jambo hilo. Yesu alikufa kwa kusudi moja, na hilo lilikuwa ni kuwaokoa wale Mungu aliotangulia kujua wangeokoka. Hiyo ni kweli. Mungu alijua kutakuweko na mtu atakayeokoka, na ilibidi kuwe na matayarisho, ama ifanywe njia wapate kuokolewa. Kama haukuweko, wokovu usingewezekana.

50 Kwa hiyo, Mungu, akitangulia kujua ya kwamba watu wangeokoka, akijua hao walikuwa ni nani, ilimbidi kufanya mpango. Sasa ungeniambia, "Ndugu Branham, basi Mungu anajua ni nani hasa atakayeokolewa?" Kweli. "Vema, kwa nini linasema, 'Yeye hapendi mtu ye yote apotee'?" Hapendi. Yeye hapendi mtu ye yote apotee, bali kwamba wote waifikie toba.

51 Lakini, kusudi awe Mungu, Yeye hana budi kujua ni nani atakayefanya hivyo, la sivyo Yeye hakuwa Mungu. Maana, Yeye ni—Yeye ni mwenye nguvu zote. Yeye anaenea kila mahali. Yeye ana nguvu zote. Anajua kila kitu. Yeye yuko kila mahali, na yuna nguvu zote. Kwa hiyo, kutangulia kujua huangalia nyuma na kusema ya kwamba Yeye alitangulia kuona jambo hili, na alijua, hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kujua mwisho ulikuwa nini, tangu mwanzo.

52 Na, kwa hiyo, tukijua ya kwamba siku hizi zote za ajabu ambazo tunaishi sasa, na kusimama na kushuhudia, na kuona mambo tunayoona sasa, ilimbidi Mungu kufanya matayarisho kwa ajili ya jambo hilo.

53 Usiku wa juzi, nilishangaa sana. Mwanamke mdogo alikuja jukwaani. Mahali pale pakubwa pa dola laki tatu pale, naye alikuwa amejipodoa kidogo usoni. Akasimama pale akaanza kutetemeka. Nikasema, "Wewe ni Mluteri," kwa Roho Mtakatifu.

Akasema, "Naam, bwana."

54 Ndipo nikasema, "Uko hapa upate kuombewa. Na sababu ya wewe kutembea jinsi unavyotembea, magoti yote mawili yalikuwa yamevunjwa." Nikasema, "Jambo hilo lilisababishwa na ajali ya motokaa, na motokaa uliyokuwa unaendesha, miaka minne iliyopita."

Akasema, "Hiyo ni kweli."

55 Nikasema, "Daktari wako ni jamaa mdogo, mfupi, mwenye upara na anavaa miwani."

Kasema, "Hiyo ni kweli."

56 Nami nikasema, “Yeye anakutibu kwa sababu mago—magotini, mfupa umeabukizwa, na hata nyama za mfupa huo zinaoza.”

Mwanamke akasema, “Hiyo ni kweli.”

Kisha akasema, “Kuna tumaini lo lote kwangu?”

57 Nikasema, “Hiyo inategemea utakavyomjia Bwana Yesu.” Nikasema . . .

Akasema, “Waweza kunisaidia?”

58 Nikasema, “La, mama. Hakuna mtu anayeweza kukusaidia sasa. Bali inakubidi kujisaidia mwenyewe kwa baraka alizotoa Mungu kwa ajili yako.”

Naye akasema, “Sasa ninaamini kwa moyo wangu wote.”

59 Nikasema, “Bwana alikuponya, dada. Ni BWANA ASEMA HIVI. Umeponywa.”

60 Akasema, “Bw. Branham, sijaweza kupiga magoti,” akasema, “kwa muda wa miaka minne.” Huku analia, amesimama pale, akisugua mikono yake. Na kusanyiko kubwa la watu wanalia, wakimwangalia; Waluteri, Wapresbiteri. Ndipo nikasema, “Mbona usishuke uende madhabahuni na kupiga magoti?”

61 Akasema, “Hebu nipige magoti papa hapa, papa hapa ambapo nimeponywa.” Hakuwa amesogeza miguu yake, bali alijua ameponywa. Kitu fulani kilitukia. Mnaona? Alijua jambo hilo. Hapakuwepo na kukisia kwo kwote.

Nikasema, “Piga magoti.”

62 Na kwa mara ya kwanza katika miaka mnne, huku magoti yote mawili yamevunjika na yana ganzi, yamefanywa, mifupa imeshikamana; mwanamke huyo, kama kijana mwanamke, alipiga magoi huku majozi yanatiririka mashavuni mwake, akainua mikono yake kwa Mungu. Vema, aliinuka moja kwa moja kutoka mahali pale, kwa urahisi tu, kama msichana mdogo, na akachuchumia akatoka jukwaani. Ilikuwa ni nini? Mungu alifanya njia kwa ajili ya jambo hilo.

63 Sasa, Yeye aliwatuma madaktari, hiyo ni kweli. Na madaktari ni sawa, nao walikuwa wamefanya yote waliyoweza. Lakini Mungu alikuwa amefanya mlango. Jambo ndilo hilo. Mnaona? Baada ya madaktari kushindwa, katika njia yake, njia ya Mungu iko juu zaidi ya njia yetu. Ni jambo la ajabu jinsi gani!

64 Sasa, kuwazia, usiku wa leo, ya kwamba wewe na mimi . . . Hutafikiri, hatutaki kufikiria jambo hili, bali kweli tumepata malezi ya kilimwengu, tuseme, kama nguruwe. Na, usiku wa leo, tumekuwa watakatifu. Jambo fulani lilipaswa kufanywa. Sasa, tusingeweza kwenda Mbinguni, kama nguruwe. Ingetubidi kwenda Mbinguni, kama watakatifu, kwa hiyo ilibidi kufanya matayarisho kwa ajili ya jambo hili.

65 Naye Mungu alitoa jambo hilo vizuri sana katika Agano la Kale. Kule nyuma katika Kitabu cha Hesabu, yapata sura ya 20, na katika Kutoka 36, 32, nasi tunaona ya kwamba kwenye siku ya Upatanisho . . . Mungu, katika mifano, akitoa kivuli cha yale angefanya, katika utimilivu wa mfano, atakapokuja, ambao ulikuwa ni Kristo.

66 Kuhani mkuu aliamriwa kuchukua mbuzi wawili, mbuzi wadogo, na kuwapeleka wawe upatanisho, sadaka, na fahali kwa ajili ya jamaa yake mwenyewe. Na wengi wenu enyi wasomaji hapa, na wasomi wa Biblia, mnajua jinsi tu ule upatanisho ulivyokuwa. Lakini basi, mbuzi mmoja . . . Ilibidi kura ifanywe. Na kura ikamwangukia mbuzi mmoja, ikafa, halafu damu ya mbuzi huyu ikawekwa juu ya yule mbuzi mwingine, huku mikono ya kuhani mkuu, akikiri dhambi za watu, juu ya mbuzi aliye hai. Ndipo mtu aliyestahili, alimchukua huyo mbuzi aliye hai chini ya mkono wake, akaenda zake jangwani ambapo huyo mbuzi ingembidi kuangamia na kuenda mahali pa upweke, mahali pa mbali. Hapana tena, katika hali hiyo, kurudi kwenye jamaa yake tena, bali atatengwa milele, akiziondolea mbali dhambi za watu.

67 Sasa, najua wanachuoni wengi, labda, wameketi hapa. Na hasa sana Wasabato, wao—wao husema ya kwamba, "Mbuzi mmoja alikuwa ni Kristo, na huyo mwingine alikuwa ni ibilisi." Sasa, ndugu, sina budi kutokubaliana kidogo na jambo hilo. Hatuwezi kumtolea ibilisi sadaka. Mbuzi hao wawili walimwakilisha Kristo. Wote wawili walikuwa Kristo. Kristo ni ninii yetu . . . Yeye alimwaga damu kwa ajili ya dhambi zetu kisha akazichukua Yeye Mwenyewe, akaziondolea mbali. Ibilisi hawezi kuzichukua dhambi zangu. Kristo ndiye mwenye kuzichukua dhambi zetu. Lifahamu jambo hilo, ndipo imani yako haitasogea. Krito ndiye mwenye kuzibeba dhambi zetu, na dhambi za ulimwengu.

68 Kristo ndiye yule mnyama aliyekuwa anakufa msalabani, sikilizeni, "Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Na mifano pekee, tulikuwa tukipata sehemu ya faida, tukijua ya kwamba utimilivu wa mfano atakuja siku moja.

69 Kwa nini alichinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia? Maana, Mungu alijua katika nia Yake, jinsi mambo hayo yangekuwa, na jinsi kanisa lingekuwa, na jinsi kila kitu kingekuwa, Naye akanena Neno. Na wakati Mungu anaponena Neno, ni kama tu limetimia, papo hapo, kwa hiyo Yeye alichijwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaliona? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

70 Unapofikia jambo hilo sasa, na kuacha imani yako itulie kwa uchaji; si juu ya mwanadamu, si juu ya theolojia za mwanadamu, si juu ya madhehebu ya kanisa, hata yawe mazuri jinsi gani, hata

mtu huyo awe mzuri namna gani. Hebu imani yako itulie pekee juu ya kazi za Kristo zilizomalizika pale Kalvari, kwa ajili ya dhambi na wokovu pia. Unaona jambo hilo?

71 Angalia, Kristo alikuja, naye alikuwa mnyama aliyekuwa anakufa, kwa maana alikuwa tayari (katika mfano) amechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Mnaliona? Mungu alinena jambo hilo na kusema ingekuwa hivyo. Kwa hiyo, wakati Mungu anaponena, limethibitishwa milele Mbinguni. Neno, lile . . .

72 Hapo ndipo unapopaswa kuwa na imani. Kama unaamini hili kuwa ni Neno la Milele la Mungu, Neno lisilobadilika, basi kila kanuni iliyonenwa katika Neno la Mungu ni Mbegu. Na kila jambo ambalo Mungu amenena, katika Neno, tayari limethibitishwa Utukufuni. Na limetolewa kwako kulitendea kazi. Kwa hiyo usiogope kuchukua sehemu yo yote ya Neno la Mungu la Milele, lililobarikiwa, na kulitia nanga moyoni mwako. Sasa, halina budi kuwa katika udongo.

73 Sasa, kwa mfano, nilichukua chembe ya ngano na kuiweka kwenye jiwe jepesi la bluu ama kitu kama hicho, labda haitakua, kwa sababu ni udongo mbaya. Lakini kama ikiingia katika udongo mzuri wa juu, mweusi na wenye rotuba, kwa hakika itakua kama ilivyowekwa mle ndani. Na wakati Neno . . .

74 Hili hapa sasa! Neno la Mungu linapoingia kwenye moyo uliojaa imani, halina budi kukua. Halina budi kushikilia. Hiyo ndiyo sababu yule mwanamke aliyesimamama pale, huku miguu yote imejaa chumvi namna hiyo, kutoka kwa yale mashapo, na kule kuvunjika kwa magoti, ambapo yote mawili yalikuwa yamepondwa, na mifupa ikaoza kwa ugonjwa, na . . . pia nyama. Hakuhofu kupiga magoti yake. Kwa ajili gani? Neno lilikuwa limeingia kwa imani. Linachipuka! Mnalipata?

75 Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alisema ya kwamba Kristo angekuwa hapa. Naye angeuawa, afe, asiye na hatia kwa ajili ya wenye hatia. Na wakati Mungu aliponena jambo hilo, lilikuwa tayari limethibitishwa wakati Mungu alipolinena.

76 Sasa, kabla halijakuwa neno, halina budi kuwa wazo, kwa maana neno ni wazo lililotamkwa. Halafu kama Mungu, katika nia Yake, aliona mambo haya, halafu yakawa katika nia Yake. Halafu, akayanena, nayo ni kama tu yamemalizika wakati Mungu anaponena, maana Yeye hawezi kukosea wala hawezi kufanya jambo lingine.

77 Halafu, nia ya Mungu. Kama Mungu aliwaokoa wenye dhambi kule nyuma, katika msingi wa kukubali sadaka ya kuteketezwa, sadaka iliyotolewa, hana budi kufanya jambo lile lile leo, la sivyo Yeye alikosea alipomchukua mwanadamu wa kwanza kwa msingi huo. Kama Mungu aliwaponya wagonjwa kule nyuma juu ya msingi wa damu iliyomwagika ya mnyama

juu ya msingi wa upatanisho, Yeye hana budi kufanya jambo lile lile leo, la sivyo alikosea alipomponya huyo mtu wa kwanza. Mnaona? Yeye hawezi kubadilika.

78 Sisi hukua. Tunakomaa. Tunaona mambo mazuri zaidi. Tunazungumza juu ya mambo mazuri zaidi. Tunavaa nguo bora zaidi, tunaendesha motokaa zuri zaidi. Tunaendelea.

79 Lakini Mungu hawezi kuendelea katika njia hiyo, kwa maana alikuwa mkamilifu kwanza. Na ukamilifu hauwezi kuendelea tena; ni mkamilifu tayari. Amina. Kwa hiyo haimbidi Yeye kusema, "Vema, huu ni wakati tofauti, tuna mawazo bora zaidi sasa." Kama ndivyo ilivyo, Yeye hawezi kuwa Mungu. Kwa hiyo, kama Yeye ni Mungu, yale aliyonena kule nyuma, hana budi kudumu nayo, kwa maana Yeye alikuwa mkamilifu huko na ni mkamilifu sasa. Mnaona? Mnaona jambo hilo? Basi, Yeye hawezi kuendelea. Hawezi . . . Vema, ninamaanisha, hawezi kuyafanya mambo yawe mazuri zaidi. Kufanya ninii hii ndogo . . . kusema, "Hii ingekuwa zuri zaidi."

Mnasema, "Na yule mwana-kondoo wa zamani, na Mwana-Kondoo huyu je?"

80 Huyo alikuwa ni mfano, kuungojea Huo, Naye alisema ulikuwa ni mfano. Yeye alinena habari za Mwana-Kondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, hapo mwanzo. "Nitaweka uadui dhidi ya Mzao wa mwanamke na Uzao wa nyoka." Halafu kungojea huo utimilifu wa wakati uje, Mungu alifanya upatanisho wa dhambi, kwa damu iliyomwagwa ya mwana-kondoo, ikielekeza.

81 Yeye alitoa jambo lile lile kupitia kwa mwezi, usiku, ukiwa mfano wa jua mchana. Mwezi ukiwa ni kivuli cha jua, ama jua likiangaza juu ya mwezi, likifanya kivuli. Mwezi na jua ni mume na mke. Na wakati jua limeondoka, linatupa nuru yake kwenye mwezi, kusudi utupe nuru kidogo mpaka jua litakapokuja. Na wakati linapokuja, mwezi hufifia.

82 Naye Kristo ni Jua Ambaye ameenda Utukufuni, akiliangazia Kanisa, kwa Nuru ya namna ile ile aliyoangaza alipokuwa hapa. Na Kanisa ni Nuru ya ulimwengu mpaka Yesu atakapokuja kisha yote iunganike pamoja. Kama vile nuru ya mwezi na nuru ya jua inavyokuwa nuru moja, wakati zinapounganika pamoja. Na wakati Kristo na Kanisa Lake watakapounganika, kwenye ule Utawala wa Miaka Elfu, wataunganika katika mmoja.

83 Na leo, "Ninyi ni Nuru ya ulimwengu." Katika Uwepo Wake . . . Asipokuwepo, hasa, Yeye anakupa Nuru ya kuangazia, anapokuwa hapa. Mambo yote ya kale, mambo yote ya dunia, ni mfano wa ya Kimbinguni.

84 Hata buibui, na mijuzi, na nyoka, na kadhalika, ni mifano tu ya pepo wachafu, wakirudisha nuru yao. Kwa nini kansa ikaitwa

kansa? Kwa sababu ina mfano wa kaa. Nalo neno *kansa* maana yake ni "kaa."

85 Sasa, mnaona, mambo hayo yote ambayo ni mifano na vivuli. Kwa hiyo, yule mbuzi wa azazeli aliyepelekwa nyikani, katika mahali pa upweke, akatengwa na wenyeji wenzake, akizibeba dhambi za watu juu ya kichwa chake, alikuwa ni mfano wa Kristo akitenganishwa na Mungu, na kutoka katika Uwepo Wake, naye akazibeba dhambi zetu hata kuzimuni. Na kule Mungu hangemtoa . . . Daudi alisema, "Sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu. Wala sikuachia kuzimu nafsi Yake." Na katika siku ya tatu, alifufuka tena tupate kuhesabiwa haki. Bali Yeye alikuwa mfano wa mbuzi, yule azazeli, na pia yule mbuzi wa sadaka ya dhambi. Mungu akifanya matayarisho, na njia iliyoandaliwa!

86 Mungu daima hufanya mlango wa kutokea, kila wakati. Magonjwa hukusukumia pembeni. Shetani hukufinyia mahali fulani unapokuwa Mkristo.

87 Labda umekuwa mcheza karata. Unaliona? Karata ziko mezani. "Endelea, Yohana, tunajua iko ndani yako." Shetani yuko hapo kukujaribu. Lakini Mungu, katika kila—kila wakati, atafanya mlango wa kutokea iwapo tu utaukubali tu.

88 Labda umekuwa m—mlevi, na glasi iko chini ya pua lako. "Naam, endelea, Yohana." Sasa, kama unataka kuisikiliza sauti hiyo, utaenda moja kwa moja kwenye matapiko yako tena.

89 Lakini Mungu daima yuko. Elekeza nia yako Mbinguni, na uangalie Kalvari, na useme, "Roho Mtakatifu aliyebarikiwa, njoo kwangu. Nina haja." Tazama kitakachotukia. Mungu atafanya mlango wa kutokea, kila wakati, kwa sababu atafanya. Mungu daima amefanya jambo hilo.

90 Na sasa angalia. Kabla ya kuangamizwa kwa ulimwengu, wakati watu walipokuwa wenye dhambi, na watu walikuwa wenye dhambi ulimwenguni, Mungu alifanya mlango wa kutokea kwa ajili ya wale wanaotaka kutokea kwake. Mungu aliagiza safina ijengwe, itayarishwe. Nuhu alijenga safina hii, kwa ajili ya kutayarisha safina hii, kwa kutayarisha mlango. Sikilizeni. Kutoka kwa . . . kwa ajili ya mlango wa kutokea, ame- . . . Hasira na hukumu ya Mungu ilikuwa ikilundikana mbinguni, kumwagwa juu ya taifa lenye dhambi na watu wenye dhambi, ambao waliukataa, na wenye shingo ngumu, wasiotii amri za Mungu. Wakati wote hasira hii ilipokuwa ikilundikana mbinguni, kumwagwa juu ya watu, katika hukumu, Mungu mwenye rehema alifanya mlango wa kutokea kwa ajili ya wale waliotaka kutokea mle. Mlango wa kutokea!

91 Sasa tumekuja kwenye mahali tena ambapo hukumu zinalundikana. Na kama siku hiyo, kabla ya ile gharika, jinsi ilivyo zaidi sana leo, wakati mwisho wa historia ya wakati, wakati wa mwisho wa historia ya mataifa, na ilikuwa ikifikia

upeo wake! Ni zaidi sana vipi hasira ya Mungu juu ya mamilioni ya watu wengi zaidi, ikilundikana pamoja, mpaka dhambi imejaa ulimwenguni, mpaka inapepesuka kama mlevi anayeyumbayumba akienda zake nyumbani kabla . . . ? . . . Tayari imepita mwezi na nyota, hata imefikia va—vazi la Yehova wa Sabato.

92 Halafu, unayumbayumba chini ya mzigo wa nadharia zake mwenyewe za kujibunia, za kujilinda, za thiolojia zake wenyewe. "Wamechukua amri za Mungu na kuzitangua, kwa kufundisha mapokeao yao ya wanadamu. Wakipenda sifa za wanadamu kuliko sifa za Mungu." Waalimu wetu walikuwa wamekuwa vuguvugu, na kuliweka juu ya kujiunga na kanisa, na kusema, "Hilo ni sawa, mradi tu wewe ni mfuasi wa kanisa. Sahau tu jambo hilo."

93 Lakini, ndugu, Mungu alifanya mlango wa kutokea. Nawe itakubidi kuja kwa masharti ya Mungu, na hiyo ni kwa njia ya Kristo Yesu Bwana wetu. Hakuna msingi mwingine uliowekwa ila ule ambao tayari umewekwa, hakuna, hakuna mwingine. Kujenga juu ya msingi mwingine wo wote, ni kama magugu na matope, mafuriko yatauchukua, na anguko lake litakuwa kubwa. Lakini Yesu alisema, "Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda." Yeye alilijenga Hilo juu ya nini? Juu ya Kweli iliyofunuliwa kiroho ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu.

"Watu hunena Mimi Mwana wa Adamu kuwa ni nani?"

94 "Wengine hunena u 'Eliya,' na wengine hunena u 'Musa,' na wengine hunena u 'Yohana Mbatizaji,' na kadhalika."

"Lakini nanyi mwaninena Mimi kuwa ni nani?"

95 Bila kusitasita, bila kuchukua sekunde moja . . . Sikiliza, ewe mwenye dhambi. Hivyo ndivyo unavyolipokea. Yeye alikuwa pamoja Naye; alijua Yeye alikuwa ni nani. Na halafu kabla hajaweza kufikiri mara ya pili, Roho Mtakatifu alimshika, akasema, "Wewe Ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

96 Kasema, "Wewe, Heri wewe Simoni, Simoni Bar-yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukujifunza hili kutoka kwenye thiolojia ya mtu fulani. Wewe hukutoka nayo kwenye seminari. Lakini Baba Yangu Aliye Mbinguni amekufunulia. Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haitalishinda."

97 Mafuriko yanaweza kuja, na atomiki zinaweza kuanguka, na kila kitu, bali yeye aliye salama katika Kristo atapanda juu ya tufani za atomiki, jinsi Nuhu alivyofanya tufani za gharika, salama kwenye safina. Hebu imani yako iingie ndani ya kitu hicho, mara moja, uone kitakachotukia; juu ya Mwamba wenye imara wa Mungu, juu ya hiyo mifano. Mungu hufanya mlango wa kutokea, kila wakati. Hana budi kufanya mlango wa kutokea. Ujapo wakati wa dharura, Mungu ni Mungu . . .

98 Yehova-yire! *Jehovah-yire* maana yake ni, "Bwana atajipatia sadaka," kwa maana Bwana atajifanyia njia ya kuepukia. Mungu anaweza kujipatia kwa sababu Yeye ni Muumba. Na Mungu, mara moja tu, pale Kalvari! Amina! Pale, pale wakati Malaika Wakuu wa Mbinguni, wakati majeshi yote ya pepo yalitetemeka, na wakati dunia ilitetemeka kwa wasiwasi na kutikisa kaburi, na wakati jua lilishikwa na msukosuko na kuning'inia kule nyuma na kugeuka likawa giza, wakati mwezi na nyota zilitikisika zikatoka mahali pao, wale waliokombolewa wa nyakati zote, na na katika nyakati zote watakuja, wataitambua saa hiyo.

99 Wakati Mwana wa Mungu alipokufa pale, alimnyang'anya Shetani kila nguvu. Hata mauti, na kuzimu, kaburi, na uoga wote, vilimezwa pale Kalvari. Wakati alipolipa ile gharama iliyo kubwa sana na wakati Mwana-Kondoo alipokufa, na dhambi ikawekwa juu Yake, Yeye alikuwa ndiye mbeba dhambi, akazipeleka kuzimuni zilikokaa. Ndipo Mungu akamfufua katika siku ya tatu. Na kwa kuamini jambo hilo, tunahesabiwa haki kwa imani, katika msingi wa Damu iliyomwagwa ya Bwana Yesu Kristo. Amina. Mungu akifanya mlango wa kutokea.

100 Loo, ndugu, unapoona ile . . . sikia gari la kubebea wagonjwa likitoa sauti, kila unaposikia moja, ni alama ya kwamba unaelekea kwenye njia hiyo. Kila unapopitia kaburini, ni alama. Unaelekea kwenye njia hiyo. Kila wakati kunyanzi linapotokea usoni, na unywele wenye mvi kichwani, ni alama. Unaelekea njia hiyo.

101 Si ajabu, basi, Paulo angweza kusema, akiwa na lile tumaini halisi lililo imara na kuimarishwa ndani yake, namna hii. Jamani! Wakati alipofikia mwisho wa safari yake, alisema, "Nimevipiga vita vilivyo vizuri. Mwendo nimeumaliza. Imani nimeilinda. Baada ya hayo, nimewekewa taji ya haki, ambayo Bwana Hakimu mwenye haki atanipa siku ile, si mimi tu, bali na watu wote wanaopenda kutokea Kwake."

102 Mbona, wewe umechukizwa na kuchoshwa na maisha haya ya kale, na utakupenda kule kufunuliwa kwa Bwana Yesu zaidi ya unavyopenda chakula chako mezani, ama mkeo, ama watoto wako, basi umewekewa taji. Si taji, taji ya dhahabu kuwekwa kichwani mwako. Bali ni mwili, usiopata maumivu, ule . . . uliotiwa taji ya Utukufu wa Mungu, uliotiwa taji ya kutopatikana na mauti kwa Yesu Kristo. Hiyo ndiyo uliyowekewa, ambayo Bwana, Hakimu mwenye haki atakupa siku ile. Hiyo ndiyo siku tunayoitarajia. Mungu amefanya mlango wa kutokea kwa ajili ya kila mmoja wetu. Bila shaka amefanya mlango.

103 Wakati nabii Danieli, mtoto wa Mungu, alipotupwa kwenye tundu la simba. Kulikuwa na wakati ambapo Danieli, akiwa mwaminifu, aliyefungua madirisha yake wala hakuhofu aliyosema mfalme. Na wakati yule . . . akaomba, bila kujali

tangazo lililotolewa, Danieli aliomba hata hivyo, huku ameelekeza uso wake Yerusalemu na kuomba. Kama watu walielekeza nyuso zao Yerusalemu na kuomba, mji ambamo dhabihu ya kuteketezwa ilitolewa . . . Hiyo ndiyo sababu Danieli aliangalia upande huo na kuomba, kwa maana Bwana tayari alikuwa amesema, "Watu wakiwa katika shida wakati wo wote, na kukabili mahali hapa patakatifu, na kuomba, basi usikie . . . Nitasikia kutoka Mbinguni," wakati Sulemani alipoiweka hekalu wakfu.

104 Hiyo ndiyo sababu Yonah alikuwa na imani aliyokuwa nayo, wakati mwani umejizungushia shingoni mwake, huku amesimama katika matapiko, katika tumbo la samaki mkubwa, kule chini kwenye kilindi cha bahari, katika bahari yenye tufani. Yeye alisema, "Huo ni ubatili wa uongo. Lakini nitatazama tena na kukabili hekalu Lako takatifu, Mungu." Mungu alifanya jambo fulani. Alimfanyia Yona mlango wa kutokea. Alichofanya, hakuna ajuaye. Hiyo ni siri ya Mungu Mwenyewe.

105 Lakini, haidhuru ni wapi ilikuwa haiwezekani, Mungu anaweza—anaweza kubadilisha hali ya mambo. Anaweza kufanya yasiyowezekana yawezekane. Na si kuwezekana tu, bali anaweza kuyafanya kitu halisi, watu wanapoliamini Neno la Mungu na kukubali njia iliyoandaliwa ambayo Mungu amemwadalia mwanadamu.

106 Mungu alifanya jambo fulani. Huenda aliweka hema la oksijeni kule. Sijui alichofanya katika tumbo la samaki huyo mkubwa, bali alimweka Yona mle kwa siku tatu mchana na usiku, kama mfano, ya kwamba Kristo angekaa bila oksijeni, katika tumbo la ardhi, na kwenye siku ya tatu atatoka tena. Ilikuwa ni mfano. Yeye alifanya mlango wa kutokea. Daima atafanya hivyo.

107 Wakati Danieli aliposimama pale, nao simba wanakuja, wanamkimbilia, hapakuwepo na uwoga katika moyo wa huyo mtakatifu mzee. Bali alisimama pale, naye Mungu hakuwa amemaliza kazi naye. Na kabla tu simba hawajamrukia, Malaika wakawaangazia mbele yao, hapana shaka bali ni Nuru ile ile ing'aayo iliyomtokea Sauli wa Tariso, akienda zake Dameski.

108 Nuru kuu ilimulika. Nao wakaangalia, wala hawakujua yaliyokuwa yanatendeka. Ndipo Sauli akaanguka kutoka kwenye farasi wake. Ndipo Sauti ikaja kutoka kwenye ile Nuru, ikisema, "Sauli, Sauli, mbona unaniudhi?"

Akasema, "Ni nani, Bwana?"

Akasema, "Mimi, Yesu, unayeniudhi."

109 Ilikuwa ni watoto Waebrania waliokuwa waaminifu kwa ahadi ya Mungu, waliokaa kule kwenye ile tanuru ya moto . . . ama Babeli, hasa, wakienda kwenye tanuru ya moto. Hatua moja kati yao na mauti.

110 Ni kiasi gani jambo hilo linaweza kuwa kwa watu hapa usiku huu. Inaweza kuwa ni siku moja kati yako na utengano wa Milele. Utafanya uamuzi wako sasa. Mlango umewekwa kwa ajili yako kama utaukubali. "Hatua moja," Yonathani akamwambia Daudi, walipotupa m—m—mshale, "hatua moja kati ya mimi na mauti."

111 Na hatua moja kati yao na mauti. Lakini katika wakati huo muhimu sana, Mungu aliandaa mlango wa kutokea, naye akamtuma Bwana Yesu Kristo katika tanuru hiyo ya moto, naye akauweka huo moto mbali nao.

112 Ilikuwa Henoko, aliyedai ya kwamba alitembea na Mungu kwa miaka mia tano na alikuwa na ushuhuda "alimpendeza Mungu." Alikuwa na imani ya kwamba "asingeona mauti." Mungu angewezaje kufanya jambo hilo? Hakukuweko na hata ndege katika siku hizo, kumwinua juu. Bali Mungu alifanya njia, kugeuzwa, ambako kulimchukua Henoko kutoka duniani hadi Utukufuni, bila kuona mauti.

113 Ilikuwa ni Eliya aliyevuka bahari. . . ama Mto Yordani siku hiyo, kwa kuigawanya kutoka upande mmoja hadi mwingine. Na wakati Eliya alipokuwa tayari kwenda Mbinguni, bila kufa, Mungu ndiye aliyemfanyia njia. Si ndege, bali Yeye alituma gari la Moto, lililovutwa na farasi wa Moto. Mungu alimwandalia njia, katika dakika moja, njia ya kuepukia kutoka mautini.

114 Ilikuwa ni Musa, ninaamini, aliyewafuata wana wa Israeli. . . ama aliyewaongoza, kufuata ile Nuru, ile Nguzo ya Moto, kupitia jangwani. Ilikuwa ni Musa aliyevumilia mpaka mwisho. Ilikuwa ni Musa, mwenye umri wa miaka mia na ishirini, baada ya miaka themanini ya kumtumikia Mungu, aliyesimama juu ya mlima na kuangalia kwenye nchi ya ahadi, huku majozi yanatiririka mashavuni mwake, ya mzee, mwenye umri wa miaka mia na ishirini. Alikuwa amepitia kwenye viwanja vya miiba. Alikuwa amepitia kwenye maji yenye kilindi. Alikuwa amenywea kikombe cha uchungu, kikombe cha siki na hofu. Alikuwa na watu wasiotii, kama mchungaji wao. Alikuwa amewaongoza kutoka mahali mahali, na kuvumilia manung'uniko yao. Na akajitupa kwenye pengo, na kusema, "Mungu, nitwae mimi kabla hujawatwaa."

115 Ilikuwa ni Musa aliyesimama pale, kama mzee, akijua ya kwamba kwa kila hali alikuwa ni mfano wa Kristo, akijua kwa vyo vyote, kwa njia fulani, Mungu hakika angemchukua, maana ilimbidi kumwinua tena, kama mfano wa Kristo. Yeye alizaliwa kama nabii, kama Kristo. Na si nabii tu, bali kiongozi, na kadhalika. Alifichwa kwenye manyasi, na vivyo hivyo Kristo alipelekwa Misri. Yeye alikuwa mtoa sheria, kama Kristo alivyokuwa kwa mlima wa Mzeituni, ambaye aliishi kutoka Sinai. Kwa kila hali, yeye alikuwa mfano wa Kristo.

116 Na wakati alipokuwa mzee, na mauti yanamkazia macho, yeye angewezaje kuleta ufufuo? Lakini wakati ule muhimu sana ulipowadia, Mungu aliandaa njia. Wakati pumzi ilipokuwa inaondoka, na kugugumia kooni mwake, aliangalia, huu hapa ule Mwamba, umesimama karibu naye. Mungu aliandaa Mwamba. Huo Mwamba ulikuwa ni Kristo Yesu ambaye alikuwa jangwani. Musa alistahimili ule Mwamba.

117 Mungu, nipe neema kuvumilia jambo lile lile. Na wakati pumzi ya maisha yangu inavutwa kutoka kwenye mwili huu, nijalie niuone ule Mwamba umesimama pale.

118 Akasimama juu ya huo Mwamba, nao Malaika wakaja wakamchukua. Miaka mia nane baadaye, yeye alikuwa amesimama kule Palestina, pamoja na Eliya, amesimama pale akizungumza na Yesu, kabla ya ule msalaba. Mungu alifanya mlango wa kutokea.

119 Mambo mawili yaliyo makubwa sana katika Agano la Kale, ninayoweza kuona katika unabii, mafarakano mawili makubwa, yalikuwa haya. Watu walikuwa wakiutazamia wakati ambao Masihi angekuja. Halafu, baada ya Masihi kuja, waliutazamia wakati, ambao Roho Mtakatifu angekuja.

120 Hatimaye, katika wakati ufaao, mifano yote kule nyuma, ambayo walikuwa nayo kupitia kwa manabii na kila kitu, mifano yote na upatanisho waliokuwa nao, hatimaye Masihi akaja, na ilikwisha kwa maana Mungu alikuwa amesema hivyo.

121 Ndipo wakautazamia wakati, wa "Kanisa kuu na lenye utukufu ambalo lingekuwa bila waa wala kunyanzi," ambalo lingeangaza duniani kama nyota. Wao waliutazamia wakati huo. Itakuwaje? Yeye alikuwa amekufa kwa muda wa siku tatu usiku na mchana. Akafufuka tena. Akawatokea watu mia tano, kisha akapaa Mbinguni. Yeye aliwaacha duniani hapa, peke yao. Hili lingekuwa ni Kanisa tukufu namna gani, wakati Kiongozi wao alikuwa ameondoka? Mungu aliahidi Kanisa. Lingekuwaje Nuru ambayo ingeng'aa mahali Pake, baada ya Yeye kuondoka?

122 Wakati aliposema pale, "Muda kidogo, na ulimwengu hautaniona tena; bali ninyi mtaniona, kwa maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yetu, hata ukamilifu wa dahari. Mambo nifanyayo Mimi. Enendeni ulimwenguni mwote mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

123 Wanawezaje kufanya jambo hilo, huku Kristo hayuko pamoja nao? Wanawezaje kufanya jambo hilo, wakati Mungu aliwapa ahadi? Lakini, angalia, Mungu aliandaa pentekoste, wakati Roho Mtakatifu, Mwenyewe, alishuka na kuchukua mwili wa bianadamu baada ya wao kusafishwa kwa Upatanisho wa Bwana Yesu Kristo. Naye Roho Mtakatifu akatwaa mamlaka juu ya mtu huyo, na kumtuma na ishara na maajabu na miujiza ikifuata. Mungu aliandaa njia. Wasingeweza kufanya jambo hilo wao wenyewe. Wao walikuwa ni wanadamu kama mimi na wewe.

Wangewezaje kufanya jambo hilo? Wasingeweza. Lakini Mungu aliandaa njia ya kuepukia.

124 Wakati walipokuwa . . . ? . . . katika chumba cha juu, walifikiri watu wangewafanyia mzaha. Walifikiri wangekuwa *hiki, kile,* ama *kinginecho*. Walikuwa wamefunga madirisha yote, na milango imefungwa. Wangefanyaje jambo hilo? Wao walikuwa waoga. Hawakuwa na uti wa mgongo. Walikuwa na uti mtamanifu wa kuku, wala si uti halisi wa mgongo wa Roho Mtakatifu. Walikuwa wamefunga milango. Walikuwa wanaogopa. Wao waliogopa kutoka nje na kukabiliana na umma. Wangewezaje kufanya jambo hilo?

125 Lakini Mungu alituma pentekoste, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kwa ghafla wakafungua madirisha na milango, nao wakaenda zao mitaani. Mungu aliuahidi. Mungu anapoahidi, Mungu atatimiza Neno Lake. Yeye atafanya mlango wa kutokea. Yeye kamwe hatawaachilia mjaribiwe zaidi ya kitu cho chote ambacho asingefanya mlango wa kutokea kwa ajili yenu. Atafanya hivyo.

126 Sisi hapa, tumeishi kupitia katika siku yenye huzuni, yenye mawingu, yenye mvua. Kanisa liko nusu ndani na nusu nje. Hawajui wanavyoweza kufanya jambo *hili,* na wanaweza kufanya nini? Wao hawakuwa na Nuru. Lakini nabii alisema, "Itakuwa Nuru wakati wa jioni." Inawezaje kuwa? Tuna . . . Kanisa katika siku hii, Kanisa hilo tukufu litakalokuwa hapa duniani, wakati Yesu ajapo kulichukua Kanisa tukufu, tunapokea mvua ya vuli, kule kumwagiwa. Sehemu maradufu ya Roho Mtakatifu inakuja duniani, na inaenea katika kila taifa, na mioto ya ufufuo inawaka juu ya kila kilima. Katika Uchina, Japan, kutoka Korea, Afrika yenye giza, na kila mahali, Roho Mtakatifu anamwagwa juu ya watu. Mungu alifanya mlango.

127 Macho yangu mapofu yaliponywaje? Mungu alifanya mlango. Haleluya! Naam, bwana!

128 Yeye daima atafanya mlango. Na kwenu ninyi hapa, mlio duniani leo, ninyi mnaongoja ile faraja, ninyi ambao ni wasafiri na wageni, iweni kama Daudi.

129 Daudi alikuwa anaenda vitani. Yeye hakuenda amefadhaika. Yeye hakuenda na alama nusu-nusu. Hakuenda akifikiri labda itafanya jambo hilo. Bali yeye alingoja kwenye vijiti vya miforsadi mpaka, baada ya kitambo kidogo, ikawa kimya kabisa, hamna kitu kinachosogea. Baada ya muda kidogo, huko nyuma kabisa, akasikia majani yakianza, sauti ikazidi kuwa kubwa, kubwa, kubwa. Baada ya kitambo kidogo, uvumi mkubwa wa upepo ukamtangulia. Alijua huyo alikuwa ni Mungu na jeshi takatifu la Malaika likimtangulia. Naye akachomoa upanga wake na kuingia vitani, akamfukuza adui.

130 Ndugu, usiruke na kufikiria jambo fulani wakati hauko tayari kwenda bado. Simama! Na uone ya kwamba si kujiunga

na kanisa, si kupeana mikono na mhubiri, wala si kubatizwa katika maji. Bali ni kukubali dhabihu iliyotolewa na Mungu, Yesu Krito, kama Mtu ndani ya moyo wako. Roho Mtakatifu atakutangulia, kama upepo uendao kasi, akiondolea mbali kila kitu. Amina. Jambo ndilo hilo. Halafu, mwe Wakristo. Ninyi mlio njiani, iweni watu wacha Mungu halisi.

131 Ufufuo utatokea hapa, karibuni sana, mkutano mkubwa wa hema. Ninaweza kuuona tu. Kweli! Unataka kufanya nini? Jiadibishe mwenyewe . . .

132 Hapa si muda mfupi uliopita, kule katika mikoa ya kusini, kulikuwa na watu waliokuwa wanaenda na kununua watumwa, na kadhalika. Imetukia tu kwamba nimekumbuka hadithi hii ndogo. Walipokuwa wakipita, wangenunua watumwa, wangeona maskini jamaa huyo alikuwa amepigwa. Wao walichukia kuiacha nchi yao, nao walijua hawatarudi. Wanegro, ni jambo la kusikitisha jinsi walivyotendwa.

133 Siku moja ikawa kwamba waliona jamaa mmoja mdogo aliyekuwa amerudisha mabega yake nyuma. Haikuwalazimu kumpiga. La, bwana. Wanunuzi fulani wakapita pale, kasema, "Hebu nimnunue mtumwa yule."

Akasema, "Hauzwi."

134 Akasema, "Vema, kwa ni kitu gani kinamfanya awe tofauti sana? Yeye ni bosi wa hao wengine?"

Kasema, "La."

135 Kasema, "Ni kitu gani kinamfanya tofauti? Unampa chakula bora zaidi?"

Kasema, "La. Yeye anakula pamoja na hao wengine." Kasema, "Ni kitu gani kinamfanya tofauti hivi?"

136 Kasema, "Ilitokea kwamba nilipata kujua ya kwamba baba yake ndiye mfalme wa hilo kabila. Ingawa yeye yuko kwenye nchi ya mbali, angali anatupa mabega yake nyuma. Yeye ni mtu aliyezaliwa kifalme. Baba yake ni mfalme. Ingawa alikuwa mgeni, babake ni mfalme.

> Baba yangu ni tajiri wa manyumba na mashamba,
> Yeye anashikilia mali ya ulimwengu mkononi mwake!
> Ya marijani na almasi, na fedha na dhahabu,
> Makasha yake yamejaa, Yeye ana utajiri usiosemeka.

137 Sisi, hawa watu hapa wa maskani hii, tuna thibitisho lisilokosea la kufufuka kwa Bwana Yesu, pamoja na ufufuo ulioenea nchini mwote; kutoka mahali padogo kama hapa, si zaidi ya lile hori la Bethlehemu, na labda padogo zaidi. Bali kupitia hapo, Mungu ametuma ufufuo mkuu, uliwavuta makumi

elfu, naam, hata kufikia mamilioni, ukawaingiza katika Ufalme wa Mungu.

138 Hivi unataka kuwa mwenyeji pamoja nasi? Uko tayari usiku huu, ewe mwenye dhambi, kutupa chini kutojali kwako, kutupa chini maisha yako yenye dhambi? Na kuyanyosha mabega yako na kujiunga na kikosi hiki cha jeshi, la watu wanaosonga mbele taratibu, tukiamini ya kwamba Upatanisho wa Bwana Yesu Kristo hutusafisha na dhambi zote.

Na tuombe, tunapoinamisha vichwa vyetu.

139 Baba yetu wa Mbinguni, usiku huu, tunapokungoja Wewe, tukimtumainia Roho Mtakatifu aliye mkuu wa Mungu kutenda kazi katika wasikizaji hawa na kufanya mambo ya ajabu mno. Kwa kuwa sasa hivi tuko tayari, tunapokaribia kufanya ushirika, Ee Baba, Mungu, tunaomba ya kwamba utanena kwa mioyo ya wenye dhambi, usiku wa leo. Hebu waje, Bwana, si kwa mwamsho hasa, si juu ya hadithi fulani ya kuhuzunisha, bali juu ya Neno la kweli la Mungu lisiloghoshiwa. "Ya kwamba Mungu aliupenda ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee, kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na Uzima wa Milele."

140 Mungu, tujalie, usiku huu, ya kwamba Maneno ya Bwana Yesu, katika Yohana 5:24, yatapiga kengele katika kila moyo. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala haingii hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Jalia wengi wapite, saa hii, kutoka mautini waingie Uzimani, tunapomngojea Roho Mtakatifu, katika Jina la Yesu Kristo.

141 Na huku vichwa vyenu vimeinamishwa. Sijui, huku dada anapocheza, kama . . . Kila mmoja, Mkristo, katika maombi. Kuna mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, ambaye ungeinua mkono wako kwa Mungu, si kwangu? Na kusema, "Sasa hivi . . . Ninainua mkono wangu, kukwambia Wewe, Mungu, ninaamini ya kwamba hukumu iko tayari kuipiga dunia. Nami niko chini ya laana ya hukumu hii. Sina budi kutenganishwa na Mungu, na Kanisa, na Wakristo. Sina budi kuteswa milele, katika kuzimu kwa Milele. Lakini, usiku huu, ninamhisi Roho Wako akinena nami, ya kwamba sina budi kuchaguliwa na Mungu. Kwa maana, Yesu alisema, 'Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba.' Nami nahisi kuvutwa kwa kipekee moyoni mwangu, hata sasa nataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wangu binafsi. Na, Mungu, ninakuinulia Wewe mkono, na kusema, kwa hili, sasa namkubali Mwanao, Yesu Kristo, dhabihu Yako iliyoitolewa, kwa dhambi zangu mbaya na dhambi zenye sifa mbaya. Sasa nainua mikono yangu Kwako." Utafanya jambo hilo?

142 Mwanamke ama mwanamume, mvulana ama msichana, aliye hapa ndani, wakati huu, ungeweza kuinua mkono wako na kusema, "Kwa huu, sasa namkubali Bwana Yesu Kristo kama

Mwokozi wangu." Ninangojea kidogo upate kufanya maamuzi. Inua tu mkono wako. Mungu akubariki, mvulana mdogo. Mtu mwingine inua mkono wako, useme . . . Mungu akubariki, ndugu yangu. Vema. Unafanya hivyo kwa Mungu, si kwangu.

143 "Wote walioamini walibatizwa, na wakaongezwa kanisani." Watu elfu tatu waliokolewa.

Kuna kisima kilichojaa Damu

144 Bila shaka. Utatumbukia sasa, kwa imani, ukisema, "Bwana Mungu, sasa najiachilia. Loo, nimeenda madhabahuni, mara nyingi. Nimefanya jambo *hili, lile,* ama nimejiunga na kanisa. Nimejaribu kuitoroka ile hasira. Lakini, usiku huu, ninakuja hivi, juu ya msingi wa kufa kwa Yesu Kristo kwa ajili yangu, Yeye alikuwa Mwana-Kondoo wa sadaka. Yeye alikuwa mbuzi wa Azazeli. Alikuwa yote. Na, katika Yeye, mimi nimekamilika. Yeye alizibeba dhambi zangu. Alichukua mahali pangu pale Kalvari. Alichukua mahali pangu chini ya hasira ya Mungu. Alichukua mahali pangu chini ya adhabu ya Mungu. Alichukua mahali pangu kuzimuni. Na kwangu mimi kuchukua mahali Pake Mbinguni, kufanyika mwana wa Mungu, sasa nakubali msingi huo sasa hivi. Kama mwenye dhambi, naamini." [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]

Wenye dhambi wanapotumbukizwa chini ya hiyo Damu,
Hupoteza mawaa yote ya makosa yao. Wanapoteza . . .

145 Iweni katika maombi, enyi kanisa, wakati mtu fulani anakata kauli kwa ajili ya Bwana. Ombeni. Anapoteza kiasi gani? Mawaa yote ya makosa yao. Myahudi, Mtaifa, mtumwa ama aliye huru, mwenye dhambi ama mufasi wa kanisa, kasisi, dacktari, mwanasheria, hata uwe nani, potezeni waa la makosa yako, kwa kumwamini Bwana Yesu, mkubali Yeye kama Mwokozi. Sikilizeni aya hii, tunapoiimba polepole sasa.

Yule mwizi aliyekuwa anakufa alifurahi kuona
Ile Chemche- . . .

146 Mwishoni mwa barabara, matumaini yote yamekwisha, kulitokea Chemchemi. Hivi umefikia mwisho, usiku huu, wa hiari yako?

Wenye dhambi wakitumbukizwa chini . . .
Wanapoteza waa lao lote la makosa.
Wanapoteza waa lao lote la makosa,
Wanapoteza . . .

147 Sasa, Baba wa Mbinguni, yote yako mkononi Mwako. Mzee na mvulana mdogo waliinua mikono yao, ya kwamba walitaka kukupokea, huku ile Chemchemi imefunguliwa kwa Neno. Tunaudhamini ushirika Wako, Bwana, Roho Mtakatifu.

148 Labda wote ni Wakristo, wote ni salama. Wewe unaijua mioyo yao, Bwana. Huenda wamevuka hata mstari ulio kati ya rehema na hukumu, wasitake tena kuinua mkono wao, ama wasitake tena kuwa na hisi yo yote ya kwamba Wewe ungewaita. Ninaomba, Baba, kama hivyo ndivyo ilivyo, uturehemu.

149 Mungu, naomba ya kwamba Wewe utamwokoa mtu huyu, Bwana. Ninaomba jambo hili sasa hivi, ndani ya roho yangu, kengele za furaha za Mbinguni zinalia. Na mvulana huyo mdogo, jinsi ile ile. Tukijua jambo hili, ya kwamba Yesu amefanya tamshi hili, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, lakini amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Hilo ni Neno Lako, Baba, nasi tunaliamini. Wape furaha ya milele sasa, ya kwamba wameukubali Uzima wa milele. Tunaomba, ya kwamba Wewe utayafanya maisha yao yajae furaha, na kuzaa matunda na yenye furaha. Tujalie, Bwana.

150 Wabariki wengine, tunapokungojea Wewe, katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

*KUFANYA MLANGO* SWA56-0304
(Making A Way)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili jioni, Machi 4, 1956, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©1996 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani  kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org